

Madarasa ya Biblia

Nehemia 8:1-3,8-12; 9:1-4 inaonyesha moja ya “madarasa makubwa ya Biblia” kupata kufanyika katika maandiko. Katika siku hiyo, “watu wote walikusanyika kama mtu mmoja,” ili kusikiliza neno la Mungu wakati Ezra akisoma na kufafanua alichokuwa anasoma, Neh. 8:3,8.

Wazee wa kanisa wanapanga na kuwezesha madarasa siku za Jumatano jioni. Ni kwa nini? Kwa nini tuwe na madarasa angalau mawili kwa juma? Kwa nini mimi na familia yangu tunatakiwa kuhudhuria haya madarasa?

Kwanza, Madarasa ya Biblia yatatufanya tumkaribie Mungu. Ndugu wa Bwana alisema, “mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.” Yohana aliyejulikana kama mtume wa upendo, aliandika katika 1Yohana 5:13 “Nimewaandikia ninyi mambo hayo ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu” Maneno ya Mungu yalitiwa wino kwa njia ya uvuvio ili kutusaidia tupate neema ya kumkaribia Mungu, kumjua Mungu na kutusaidia “kulifahamu pendo la Mungu,” 1Yohana 3:16. Na madarasa ya Biblia ndiyo nyenzo isiyokanika kwamba hutusaidia kukua katika kumkaribia Mungu kila uchao.

Pili, madarasa ya Biblia hutupatia lishe ya kutuimarisha. Ndani ya sentensi ya mwisho, twaona mambo mawili ambayo neno la Mungu hufanya. Neno hutuboresha na kutustawisha (Zaburi 1:1-6; Yohana 17:20-23; 2 Petro 3:18; Mathayo 4:4).

Ninapofikiria juu ya familia yangu na mimi, kama mtunzaji, nataka kuwapatia wanangu kitu ambacho kitawakuza na

kustawisha. Nataka wapate mlo bora kwa kadri iwezekanavyo kitachowasaidia kukua na kurefuka na kuwa na nguvu. Pia, nataka kuwapatia kilicho bora zaidi! Na ni wazi kuwa elimu nzuri ya Biblia ndiyo bora kabisa. Na ingawa kanisa hutupatia madarasa ya Biblia, tusipuuze yale tunayopaswa kuyafundisha majumbani bali iwe nyongeza wa yale tunayofundisha majumabani. Madarasa ya Biblia hutolewa ili kuwasaidia watoto wetu, kama Timotheo “kukuhekimisha hata upate wokovu” (2 Timotheo 3:15), tangu utotonii.

Neh.9:7-38